# LEARNING BY EAR 2010

## SHALL I TELL YOU SOMETHING?

## AFRICAN FABLES FOR A CULTURE OF PEACE

**EPISODE 9: „THE MOST BEAUTIFUL OF ALL“**

**AUTHOR:** IBRAHIMA NDIAYE

**EDITORS:** YANN DURAND, STEFANIE DUCKSTEIN, NAÏMA GUIRA

**TRANSLATION:** NATALIE GLANVILLE-WALLIS

**PROOFREADING:** TONY DUNHAM

**KISUAHELI :** ERIC PONDA

*Sound Clips: liegen bis Mitte Juli vor*

**CHARACTERS:**

1. NARRATOR (male, 40 years old at least)
2. PEACOCK (male, about 20)
3. MARABOU (male, about 30)
4. PARROT (female, about 20)
5. SPEAKER FOR ONE SENTENCE (female, age irrelevant)

**INTRO:**

Hujambo msikilizaji na karibu kwa makala ya tisa kwenye mfululizo wa vipindi vya “Noa Bongo! Jenga maisha Yako” tukiwa bado katika maada ile ya “JE NIKUDOKEZEE”, hizi zikiwa ni ngano za Kiafrika kuhusu utamaduni wa kudumisha amani na maridhiano. Katika kipindi cha leo tunazungumzia suala la majivuno. Kwanini majivuno hayafai na jinsi yalivyomuadhibu Tausi. Endelea kusikiliza hadi mwisho.

1. **MUSIC (plays in background for the entire script)**

2. **NARRATOR:**

Miaka mingi tu iliyopita, palitokea Mungu Bigolo aliyewaumba ndege na kisha kuwatuma duniani. Ndege hao walitarajiwa kudumisha na kukuza amani. Wakati huo, kuku bado alikuwa na meno yake huku Tausi naye akiwa mweupe kama chumvi. Waliishi pamoja kwa furaha, na kulikuwa na chakula cha kuwatosha. Lakini
Ndege Kongoti ambaye alikuwa amefanywa kuwa mfalme wa wote akawaita na kuwahutubia.

3. **MARABOU:**

“Ndugu na Dada zangu, ni wazi kwamba tumetumwa hapa duniani kwa lengo fulani. Na kwa mara ya kwanza kabisa tumeachwa kujitegemea. Kwa hakika Mungu ndiye tu ajuaye hatima yetu. Hata hivyo lakini, tuna jukumu la kujisimamia na kuhakikisha kuwa tunaishi pamoja kwa amani. Hivyo nawatakia kila la kheri katika maisha yenu mapya.”

**4. SFX:** ***Fluttering of wings and bird cries***

**5. NARRATOR:**

Na alipokamilisha hotuba yake, mfalme huyo akaondoka. Kila mmoja alikuwa uhuru kuendelea na alichokuwa akifanya kwa raha zake. Maisha yalikuwa mazuri sana na kila mmoja aliyafurahia, hadi pale msimu wa baridi kali ulipoingia katika shamba hilo. Baridi iliathiri mambo mengi na kubadili kabisa mpangilio wa maisha katika shamba hilo. Tausi ambaye alikuwa na manyoya mepesi ndiye aliyeathirika zaidi, kwani hangeweza kustahimili baridi hiyo kali. Na alitetemeka kama majani ya mti kutokana na baridi hiyo kali.

**6. SFX:** ***Chattering beak (by the peacock actor)***

**7. NARRATOR:**

Alianza kukohoa bila ya dalili za kupona na hapo, Tausi akaamua kwenda kumuona Mfalme Kongoti, angalau apewe hifadhi na ushauri pia.

**8. PEACOCK** ***(still chattering, trembling voice):***

"Tafadhali mfalme nihurumie. Siwezi kustahamili baridi kali iliyoko huko nje. Hata nimeanza kuwa na harahara kwa sababu ya baridi. Kama hutanisaidia, huenda nikapatwa na jambo baya zaidi katika muda usio mrefu."

**9. NARRATOR:**

Kwa huruma, Mfalme Kongoti akamuagiza msaidizi wake kasuku kuitisha mkutano mkubwa. Na walipomuona Tausi, wote walimuonea huruma. Ombi la Mfalme kumsaidia Tausi likaridhiwa na wote kwa kauli moja na wakatoa msaada wa blanketi kila mmoja. Kisha wakamzingira na kuanza kumbandika manyoya mwili wote kwa kutumia gundi kutoka kwa mbuyu. Baadaye kila mmoja alirejea nyumbani huku Tausi akijisikia nafuu kutokana na msaada huo. Wiki chache baadaye, msimu wa joto ukaingia, jua likaanza kuwaka na kusababisha joto jingi. Ili kusherehekea msimu huu, Mfalme aliamua kuitisha tena mkutano mwengine. Na kama ilivyo desturi, Kasuku aliagizwa kusambaza habari hizo kwa jamii nzima. Na bila kuchelea akabisha nyumba hadi nyumba kutoa mwaliko huo.

**10. PARROT: *Repeated cries***

**11. PARROT:**

“Shukrani kupata tena msimu wa Joto. Sasa Mfalme anamualika kila mmoja kufika katika makao yake ili kusherehekea hali nzuri ya hewa. Tushukuru kurejea kwa msimu huu wa joto!”

## 12. NARRATOR:

Hata Tausi ambaye bado alikuwa amelala alipata fununu ya habari hizo njema. Siku iliyofuata, kila mmoja alifika katika kasri ya Mfalme ispokuwa Tausi ambaye kwanza alikwenda mtoni kuoga na kujitayarisha ili kurudisha hali yake ya kawaida. Na alipokuwa akijiandaa kutosa kichwa chake mtoni, akaona kivuli chake na akashtuka sana kwa jinsi alivyokuwa. Ghafla alijiona amegeuka na kuwa mrembo kupindukia. Urembo ambao ameweza kuhifadhi hadi leo. Manyoya yake yalikuwa yamegeuka rangi nyingi nyingi tu. Kishungi cha rangi ya samawati mfano wa kichana, pia kilikuwa kimeanza kumea kichwani mwake. Akaoga taratibu kisha akaanza kulainisha manyoya yake ya kumeremeta huku akiota jua.
Baada ya kuridhika na urembo wake, akaenda moja kwa moja hadi eneo la sherehe ambako tayari sherehe zilikuwa zimenoga. Na alipojitokeza tu kila mmoja aligutuka na kumtazama Tausi kwa alivyochelewa. Lakini zaidi walishangzwa na urembo wake.

## 13. SFX: *Bird cries and fluttering of wings suddenly stop (people talking and some bird cries in the studio?)*

## 14. PARROT:

"Kweli huyu ni Tausi?"

**15. SPEAKER:**

"Mbona amekuwa mrembo hivi?"

**16. PARROT:**

"Tushukuru kuwa na msimu wa joto!"

**17. NARRATOR:**

Kila mmoja alikuwa akimzungumzia Tausi. Ndege wote wakasisimka. Na huku akijimwaya mwaya kujivunia urembo wake, na kujiona bora zaidi kuliko wengine, Tausi alichukua fursa hiyo kuonyesha urembo wa manyoya yake na kutembea kwa madaha kwenye jukwaa kana kwamba anakagua gwaride la heshima. Akijidai kuomba msamaha, Tausi aliinama kumpa heshima mfalme kisha kugeukia umma na kuanza kuhutubu bila ya hata samahani.

**18. PEACOCK:**

"Asanteni nyote, sasa najihisi mrembo zaidi kuliko wote. Na kuanzia leo ningependa mniite Mansa Dibon, mfalme wa mwituni."

**19. SXF: *EVERYONE TALKING ANGRY TO EACH OTHER (actors)***

**20. NARRATOR:**

Kiburi chake kiliwaudhi wote waliokuwa wamemsaidia na blanketi wakati wa msimu wa baridi. Lakini Tausi hata halikumgusa akaendelea na madaha yake yaliyozidi kuwaudhi wenzake. Hivyo, baadhi ya ndege wakaamua kumfuchua manyoya yote Tausi. Hapo Mfalme akasimama kutoka kiti chake cha enzi ili kuingilia kati kuzuia fujo hizo.

**21. MARABOU:**

Ama kwa hakika Tausi umependeza, lakini wewe ovyo, huna shukrani. Kwa taarifa yako, haya majivuno hayawezi kukufikisha mahali popote. Mungu pekee ndiye anayeweza kuamua hatima yako. Na sherehe hizi sasa zimefika kikomo kila mmoja arudi kwake nyumbani!

**22. NARRATOR:**

Siku iliyofuatia, asubuhi na mapema, kwa mara ya kwanza kabisa Mungu akatengeneza upinde wa mvua. Ndege wote wakakimbilia mtoni kutafakari sanaa hii ya ajabu.

**23. *SFX: Rush, fluttering of wings, peeping, chattering***

**24. NARRATOR:**

Kwa msisimko ndege hao walipiga piga mbawa zao, kuruka ruka na kuimba kwa furaha. Na hapo Tausi akawasili na kuanza kuona wivu kwa jinsi upinde wa mvua ulivyopendeza. Alijaribu kupambanua manyoya kwenye mkia wake, lakini hakuna yoyote aliyeshuhgulika naye. Baada ya kuhisi amepuuzwa akaanza kulia kwa sauti iliyopwelea .

**25. PEACOCK: *Hoarse cry***

**26 NARRATOR:**

Lakini wapi, kinyume kabisa na alivyodhamiria, sauti yake iliharibika kabisa isirudi tena. Na tangu wakati huo amesalia kuwa ndege wa kupendeza lakini mlio wake humfanya kila mmoja kutoroka.

*Na hadi hapo ngano yetu inafika ukingoni, na wa kwanza kuvuta harufu yake, bila shaka ataiona mbingu.*

**27. Music**

**OUTRO:**

Na hadi hapo msikilizaji tunafika mwisho wa ngano yetu "Uzuri kushinda vyote." Ngano ambayo mwisho wake umekuwa wa kuhuzunisha. Majivuno ya Tausi ambayo mwishowe yalimponza. Lakini yote hayo ni makosa yake kwa sababu ya ufidhuli wa kutaka sifa. Je, unadhani wanyama wengine walimuonea? Tafadhali tuandikie barua pepe kwa kutumia anuani hii lbe@dw-world.de. Pia unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki au vipindi vingine vya Noa Bongo kupitia mtandao wetu www.dw-world.de/lbe. Shukrani kwa kuwa nasi, hadi wakati mwengine tutakapokutana tena kwaheri kwa sasa!

END